

COUNTY GOVERNMENT OF LAMU



THE COUNTY ASSEMBLY OF LAMU

THE HANSARD

Tuesday, 27th February, 2024

*The Assembly met at the
Main Chambers, at 2:30 p.m.*

[Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna) in the Chair]

PRAYERS

Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna): Next Order.

Clerk-at-the-Table: Papers.

PAPERS

MCA Hope Wanjiku Mwaura (Nominated): Thank you Mr Speaker.

Mr Speaker Sir, I beg to lay the following paper on the floor of this House:-

1. Report of the Trade, Tourism, Information and Cooperative Development Committee.

Thank you.

NOTICE OF MOTION

MCA Hope Wanjiku Mwaura (Nominated): Thank you Mr Speaker.

Mr Speaker Sir, I beg to give the following Notice of Motion:-

APPROVAL OF THE REPORT OF THE TRADE, TOURISM, INFORMATION AND COOPERATIVE DEVELOPMENT COMMITTEE ON THE VETTING OF THE CHIEF OFFICER NOMINEE FOR CLIMATE CHANGE, ICT, AND E-GOVERNMENT , MR ALI AHMED MUHDHAR.

That, pursuant to the provisions of the Constitution of Kenya , County Governments' Act No 17 of 2012 and the County Assembly's Standing Orders, this County Assembly approves and adopts the report of the Trade, Tourism, Information and Cooperative Development Committee on the vetting of the Chief Officer nominee for climate change, ICT and E-Government, Mr Ali Ahmed Muhdhar, laid on the table of the House today, Tuesday, 27th, February 2024.

Thank you.

Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna): Next Order.

Clerk-at-the-Table: Motion.

MOTION

MCA Hope Wanjiku Mwaura (Nominated): Thank you Mr Speaker.

Mr Speaker Sir, I beg to move the following Motion:-

COUNTY SCHOLARSHIP REGULATIONS

Aware that, The Constitution of Kenya 2010 Article 56(b) reads that, " The State shall put in place affirmative action programmes designed to ensure that minorities and marginalized groups-“ Are provided special opportunities in Educational and Economic fields;”

Further aware that, Article 43(f) states that every person has the right to education. Article 439(C) reads that “ The State shall provide appropriate social security to persons who are unable to support themselves and their dependants”.

Concerned that, the Lamu County Scholarship programme was initiated and implemented based on 300 marks as a minimum thresh hence as requirement without considering social conscience as the best year stick for determination and without guidelines or regulation to govern Lamu County Bursary Act.

Seriously concerned that, students who are abled differently, partial and total orphans have had numerous challenges on their way towards attaining 300 pass marks and C in their terminal exermination in schools, subjecting both the guardians and the candidates psychological problems. Some students have droppede out of school due to inability of parents to pay school fees.

I urge this Assembly to compel, the County Executive Department in charge of Education to come up with regulations on the acholarships that will give criterions of beneficiaries, pass mark among others into the full scholarship programme.

Thank you.

(seconded)

(Motion proposed)

(Members contributions)

MCA Mohamed Aboud Abubakar (Faza): Asante Mheshimiwa Spika, ningependa kuchangia kuwa, mwongozo ni muhimu na itakuwa bora zaidi ikiwa sisi tutatia mkazo kusaidia serikali kuleta mwongozo mzuri ili watoto wanaofadhiliwa waweze kusoma bila matatizo haswa kwa wale wanaoacha kusoma kwa sababu ya kushindwa kulipa karo.

Inaskitisha sana kwa wale watoto waliotolewa katika ufadhili huu kwa sababu ya kushindwa kufikisha ile alama iliyoamuliwa na serikali yetu ilhali watoto hawa

hawana wazazi wala usaidizi mwengine wowote kwa hivyo, nimejaribu kuongea na waziri pamoja na wahusika ili waendeleo kulipiwa kwa sababu hawajiwezi.

MCA Suleiman Mohamed Farah (Witu) : Mheshimiwa Spika kusema kweli, ufadhili wa kielimu katika kaunti yetu ya Lamu hauna muongozo mzuri kwa sababu tulipitisha bajeti ya vijana hawa lakini nashangaa wakisema mzazi alipe nusu. Kwani ile pesa tulipitisha imeenda wapi? Wazazi ama watoto hawa hawana uwezo wa kuja katika bunge hili kutafta usaidizi ndiposa wakatuchagua sisi kama viongozi kuja kuwatetea.

MCA Aisha Ali Abdulrahman (Nominated): Asante Mheshimiwa Spika, ningependa kuchangia kuwa, kuna sehemu za mashambani ambapo watoto hawaezi kufikisha alama 300 na ni watoto wasioweza kujikimu katika maisha. Watoto kama hawa wakiweza kufadhiliwa itakuwa tumewasaidia pakubwa. Vile vile kuna watoto mayatima wanaoathirika katika masomo yao kwa sababu ya ukosefu wa malezi na maisha ambayo wanachangia kutofikisha alama 300. Kwa hivyo kupitia kwako, naomba mswada huu upitishwe ili uweze kujumlisha watoto wote.

MCA Rebecca Wainaina (Nominated): Nashkuru Bwana Spika kuleta kunipatia fursa hii kuchangia kwa sababu hili ni jambo muhimu linalotakikana liangaliwe kwa makini. Kusema kweli, kila mzazi anatamani mtoto wake asome na kila mwanafunzi anatamani asome na amaliza. Kwa hivyo kukiwa namuongozo wa jinsi ya kuwapa watoto ufadhili huu wa kielimu takuwa ni muhimu sana hususan wale wasiojiweza kujikimu kimaisha. Kuna baadhi ya wanafunzi wanasoma huku wanajishughulisha na vibarua ili waweze kujisomesha. Baadhi yao kuanguka katika masomo si kutaka kwao. Huenda ikawa mwanafunzi alikuwa bora alafu akaja kuanguka katika mtihani wake wa mwisho kwa sababu ya ugonjwa ama msongamano wa kimawazo. Mwaka huu huu nimeshuhudia kesi ambayo mzazi ni mlemavu na mtoto ndiye amebeba majukumu ya familia hio huku akijisomesha. Watoto kama hawa wanafaa waangaliwe kwa sababu wana mahitaji muhimu.

MCA Beatrice Wamaitha Munge (Nominated) : Thank you Mr Speaker Sir, the children of Lamu county have the right to education as per the Constitution. There are some students who hardly attain 300 marks due to some unavoidable circumstances. We need to know on how we can accommodate these children without demoralising them as they are all equal. It is very sad when we see such children loitering on the streets as later on they are going to sit for the same end examination with those that have been attending their classes.

MCA Shekhuna Abbas Shekhuna (Mkomani) : Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha sana ikiwa sisi viongozi tutanyamaza tuonapo ona watoto wanajizungukia kisa ni ukosefu wa karo. Mheshimiwa Spika, ningependa kuuliza mwenyekiti wa ni sisi tulipitisha kwa bunge ama ni afisi ya utendakazi? Haswa watoto mayatima ni muhimu waweze kupata msaada wa ufadhili huu na wasitolewe katika ufadhili ili aweze kupata motisha. Viongozi wenzangu ningependa tushikane ili tuweze kuwasaidia watoto hawa na jambo hili lisicheleweshwe.

MCA Barisa Deko Bana (Basuba) : Mheshimiwa Spika, ni wakati wa bunge hili kusimama na wananchi wake kwa sababu sisi kama viongozi, ni jukumu kuwatumikia wananchi hawa. Ni sikitiko kubwa kwa watoto 700 kutolewa katika ufadhili huu. Kaunti yetu haiwezi kuwa na maendeleo ikiwa tutaendelea hivi. Tunafaa tuwamiliki watoto hawa kwa sababu tukiangalia nchi yetu, tumeringizwa na maafa makubwa sana. Bunge lina uwezo wa kuwamudu watoto wote na si lazima mtoto afikishe alama 300. Naomba Bunge hili letu liweze kushughulikia swala hili haraka ipasavyo kwa sababu tutawakosa watoto hawa wakianza kuzurura mitaani.

MCA Mercy Wangeci Nyambura (Nominated): Thank you Mr Speaker Sir, we, as ward representatives, we have seen that there are so many concerns about scholarships and bursaries and it is high time that we need to take action on this.

MCA John Mburu Gitonga (Hongwe): Asante Bwana Spika, ningependa kuunga mkono kwa sababu mahali naishi ni karibu na shule, na watoto wakifukuzwa huwa nashuhudia. Kama tunavyoona, maisha yako juu na watoto wanashindwa kulipa karo. Kwa hivyo naomba kuwe na mpangilio mzuri kuhusiana na jinsi ya kutoa ufadhili huu na pia mswada huu upitshwe kwa haraka kwa sababu watoto hawa wapate kusaidika.

Mover's Response

MCA Hope Wanjiku Mwaura (Nominated): Asante sana Bwana Spika, pia ningependa kuwapongeza Viongozi wenzangu kwa kuunga mkono mswada kama huu ambao utaweza kuwasaidia watoto wetu kwani, hakuna kitu kitasawazisha mtoto wa maskini au tajiri kama elimu bora. Inaskitisha kuskia vilio vya watu wetu kila mara kwa sababu ya ufadhili ambao hauna mpangilio mzuri. Mimi binafsi nimepitia ile 'Bursary Act' na hakuna mahali imeandikwa kuwa mzazi anafaa kujijazia nusu yake. Kuna familia ambazo hazijiwezi na wanalemewa na maisha hivyo basi kushindwa kulipa karo. Naomba wahusika waandike muongozo kwa vizuri ambao wataweza kuwabeba watoto wote wanaopitia hayo.

(Question put and agreed upon)

ADJOURNMENT

[Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna)]: Honorable Members, there being no other business, the Assembly stands adjourned until Tomorrow, 28th February, 2024 at 10:30 a.m.

The Assembly rose at 3:30pm